GREDI YA SITA - 2026
KISWAHILI

6

Jina:.....

Shule: .....

Gredi: ..... Tarehe:.....

Jibu maswali yote.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1-5.

(Ni wikendi wanafunzi wamentembelea daktari hospitalini)

Wanafunzi	:	Shikamoo daktari!
Daktari	:	Marahaba wanafunzi. Masalkheri?
Wanafunzi	:	Akheri.
Julia	:	Jina langu ni Julia. *(Akiashiria Salim)* Mwenzangu anaitwa Salim.
Daktari	:	***(Akitabasamu)*** Naam, Julia na Salim.
Julia	:	Sisi ni wanafunzi wa shule ya msingi ya Daima. Vilevile, sisi ni viongozi wa kilabu cha afya shuleni mwetu.
Salim	:	Tumekutembelea ili utufunze kuhusu afya ya akili ili turudipo shuleni, tuwahamasishe wenzetu vilevile.
Daktari	:	Asanteni kwa kuja ofisini mwangu. Je, mnajua maana ya afya ya akili?
Salim na Julia	:	Hapana.
Daktari	:	Afya ya akili ni hali ya kuwa sawa kimawazo, kitabia na kihisia na kuweza kutatua changamoto za maisha kwa njia inayofaa.
Salim	:	Samahani daktari. Unamaanisha kuwa mtu akiwa na maradhi ya akili amekosa afya ya akili?
Daktari	:	Ndiyo. Kwa sasa nawaomba mrudi nyumbani na kurudi wikendi ijayo ambapo nitawapa maelezo zaidi. Nataka kumwona mgonjwa mmoja ambaye ako katika hali mahututi.
Salim na Julia	:	Asante daktari.

1. Mazungumzo haya kati ya wanafunzi na daktari yalifanyika wakati gani?
   (A) Asubuhi (B) Mchana
   (C) Jioni (D) Usiku

2. Wafuatao ni wahusika katika mazungumzo haya isipokuwa:
   (A) Daktari (B) Maria
   (C) Salim (D) Julia

3. Sababu kuu ya Salim na Julia kumtembelea daktari ni _____.
   (A) Ili waweze kutibiwa.
   (B) Ili awafunze kuhusu afya ya akili.
   (C) Kumtembelea mwanafunzi mgonjwa
   (D) Kwa sababu walikuwa wametumwa na mwalimu mkuu

4. Ni nini kinyume cha neno **akitabasamu** lililotumika katika mazungumzo?
   (A) Akinuna (B) Akicheka
   (C) Akilia (D) Akifurahi